Tume ya Taifa ya Uchaguzi

Maamuzi ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi kuhusu Rufaa

Tume ya Taifa ya Uchaguzi imepokea jumla ya **rufaa 54 za madiwani** kupinga Maamuzi ya Wasimamizi wa Uchaguzi katika majimbo mbalimbali nchini. Pia jumla ya rufaa **198 za madiwani** kutoka Halmashauri mbalimbali.

Tume imeanzakupitia vielelezo vilivyowasilishwa na Wagombea (warufani) na Wasimamizi wa Uchaguzi kutoka majimboni. Imeanza kuzitolewa maamuzi rufaa za Wabunge. Leo tarehe 31/82015 zimejadiliwa na kuamuliwa rufaa 38. Zilizobaki mawasiliano yanaendelea kati ya Tume na Wasimamizi wa Uchaguzi ili kupata vielelezo vinavyohusika kuisaidia Tume kufikia maamuzi ya kisheria na haki kwa wagombea na vyama vyote vinavyoshiriki katika uchaguzi.

Wagombea waliokuwa wamewekewa pingamizi na **kuenguliwa na Wasimamizi wa Uchaguzi ni 16** na Tume **imerudisha wagombea 13** kati ya hao, waliobaki ni 3 ambao Tume imeridhia maamuzi ya Wasimamizi wa Uchaguzi. Hii ni kutokana na vielelezo vilivyowasilishwa kutoonesha makosa ya kisheria au kiufundi.

Na.	Jimbo	Mrufani	Mrufaniwa	Sababu za rufaa	Uamuzi wa Tume
1	Rungwe	Frank George Maghoba ACT Wazalendo	Saul Henry Amon CCM	Hakuridhika na uamuzi wa Msimamizi wa Uchaguzi, pingamizi alilomwekea Mgombema wa CCM	Tume imekataa rufaa na wagombea wote wanaendelea na kampeni za uchaguzi.
2	Kinondoni	Karama Masoud Suleiman, ACT Wazalendo	Azzan Iddi Mohamed CCM	Kwamba Tume ikubali kuwa alidhaminiwa na Chama cha ACT Wazalendo na kumrejesha katika orodha ya Wagombea.	**Tume imekubali Rufaa na kumrejesha Mgombea wa ACT Wazalendo katika orodha ya Wagombea wa Jimbo la Kinondoni**
3	Peramiho	Mwingira Erasmo Nathan CHADEMA	Jenista Joakim Mhagama CCM	Kwamba Tume ione kuwa aliwasilisha tamko la kisheria na tamko la kuheshimu Maadili kwa mujibu wa sheria	**Tume imekubali Rufaa na kumrejesha Mgombea wa CHADEMA katika orodha ya Wagombea wa Jimbo la Peramiho.**
4	Lindi Mjini	Barwany Salum Khalfan CUF	Kaunje Hassani Selemani CCM	Tume ikubali kuwa Muhuri uliotumika ni wa Mtendaji wa Chama badala ya Muhuri wa Chama. Kuwa alipaswa kudhaminiwa na chama na siyo mtendaji wa chama.	Tume imeikataa rufaa kwa kuwa muhuri uliotumika ni wa CCM, hivyo mrufaniwa ametimiza matakwa ya kisheria.

5	MLALO	GOGOLA SHECHONGE GOGOLA (CUF)	RASHID ABDALLAH SHANGAZI (CCM)	Tume ikubali kuwa tamko la mrufani ni kwa mujibu sheria	**Tume imekubali Rufaa na kumrejesha Mgombea wa CUF katika orodha ya Wagombea wa Jimbo la Mlalo.**
6.	MAFIA	KIMBAU OMARY AYOUB (CUF)	DAU MBARAKA KITWANA (CCM)	Si raia wa Tanzania.	Tume imeikataa rufaa kwa kuwa hakuna ushahidi kuwa mrufaniwa siyo raia wa Tanzania.
7.	MJI WA HANDENI	DAUDI KILLO LUSEWA (CHADEMA)	KIGODA ABDALLAH OMARI (CCM)	Hakudhaminiwa na wapiga kura walioandikishwa katika jimbo.	**Tume imekubali Rufaa na kumrejesha Mgombea wa CHADEMA katika orodha ya Wagombea wa Jimbo la Mji wa Handeni.**
8.	NJOMBE KUSINI	EMMANUEL GODGREY MASONGA (CHADEMA)	EDWARD FRANS MWALONGO (CCM)	1. Hana sifa za kwasababu Mgombea Ubunge. 2. Ametiwa hatiani kwa kosa la kukwepa kulipa Kodi katika kipindi cha miaka mitano kabla ya Uchaguzi.	Tume imeikataa rufaa kwa kuwa hakuna ushahidi kuwa mrufaniwa alitiwa hatiani.
9	NJOMBE KUSINI	EMMANUEL GODFREY MASONGA (CHADEAMA)	WILLIAM EDWARD MYEGETA (DP)	1. Si Raia wa Tanzania. 2. Hana sifa za kuwa mgombea Ubunge.	Tume imeikataa rufaa kwa kuwa hakuna ushahidi kuwa mrufaniwa si raia wa Tanzania.

10.	NJOMBE KUSINI	EMMANUEL GODFREY MASONGA (CHADEMA)	EMILIAN JOHN MSIGWA (ACT - wazalendo)	1. Si Raia wa Tanzania. 2. Hana sifa za kuwa mgombea.	Tume imeikataa rufaa kwa kuwa hakuna ushahidi kuwa mrufaniwa si raia wa Tanzania.
11.	KINONDONI	KALUTA, AMIRI ABEDI (CHAUMMA)	AZZAN IDD MOHAMED (CCM)	Hakudhaminiwa na Chama cha Siasa kugombea Ubunge.	Tume imeikataa rufaa kwa kuwa mrufani (mgombea) wa CHAUMMA alijithibitisha na kujisainia fomu za Uteuzi mwenyewe kinyume cha sheria. Tume imekubaliana na uamuzi wa Msimamizi wa Uchaguzi wa kumuengua katika kinyang'anyiro cha Ubunge katika Jimbo la Kinondoni.
12.	MICHEWENI	KHAMIS JUMA OMARI (CCM)	HAJI KHATIB KAI (CUF)	Si raia wa Tanzania	Tume imeikataa rufaa kwa kuwa hakuna ushahidi kuwa mrufaniwa si raia wa Tanzania. Hivyo Tume imekubaliana na uamuzi wa Msimamizi wa Uchaguzi.
13.	CHALINZE	SHOO GASPER AIKAELI (ACT – Wazalendo)	KIKWETE RIDHIWANI JAKAYA (CCM)	1.Hana sifa za kuwa Mgombea Ubunge 2.Hakurudisha fomu za uteuzi kwa mujibu wa masharti yaliyowekwa na Sheria.	**Tume imekubali Rufaa na kumrejesha Mgombea wa ACT Wazalendo katika orodha ya Wagombea wa Jimbo la Chalinze.**
14.	CHALINZE	TORONGEY	KIKWETE	Hakurudisha Fomu za Uteuzi	**Tume imekubali Rufaa**

		MANGUNDA MATHOYO (CHADEMA0	RIDHIWANI JAKAYA (CCM)	kwa mujibu wa masharti yaliyowekwa na Sheria.	**na kumrejesha Mgombea wa CHADEMA katika orodha ya Wagombea wa Jimbo la Chalinze.**
15.	KASULU MJINI	MACHALI MOSES JOSEPH (ACT – Wazalendo)	NSANZUGWANKO DANIEL NICODEMUS (CCM)	Hajatimiza umri wa miaka 21 Hana sifa za kuwa Mgombea Ubunge	Tume imeikataa rufaa kwa kuwa kosa la kuandika tarehe ya kuzaliwa kuwani 15.08.2015 katika fomu moja dhidi fomu 3 zilizoandikwa kwa usahihi, hili haliwezi kuwa kosa la kumuondolea sifa za kuwa mgombea. Hivyo Tume imekubaliana na uamuzi wa Msimamizi wa Uchaguzi na Mrufaniwa anaendelea kuwa mgombea halali.
16.	MWANGA	KILEWO HENRY JOHN (CHADEMA)	PROF. MAGHEMBE JUMANNE ABDALLAH (CCM)	1. Hakudhaminiwa na Chama cha Siasa kugombea Ubunge 2. Hakuwasilisha tamko la Kisheria	Tume imeikataa rufaa kwa kuwa mrufaniwa amedhaminiwa na CCM. Aidha, alitoa tamko la kisheria. Hivyo Tume imekubaliana na uamuzi wa Msimamizi wa Uchaguzi kuwa Mrufaniwa ni mgombea halali.
17.	Tarime Mjini	Esther Nicholas Matiko	Deogratius Meck Mbagi	1 .Hakudhaminiwa Na Chama Cha Siasa Kugombea Ubunge.	Tume imeikataa rufaa kwa kuwa mrufaniwa ametimiza sharti la kiapo cha kisheria na tamko la kuheshimu na

		(CHADEMA)	(ACT – Wazalendo)	2.Hakuwasilisha Tamko La Kisheria. 3. Hakutoa Tamko La Kuheshimu Na Kutekeleza Maadili Ya Uchaguzi Ya Mwaka 2015.	kutekeleza Maadili ya Uchaguzi. Hivyo Tume imekubaliana na uamuzi wa Msimamizi wa Uchaguzi kuwa Mrufaniwa ni mgombea halali.
18.	Ulanga	Celina Ompeshi Kombani (CCM)	Ikongoli Pancras Michael (CHADEMA)	1. Hawezi kusoma na kuandika. 2.Hakudhaminiwa Na Chama Cha Siasa Kilichosajiliwa.	Tume imeikataa rufaa kwa kuwa mrufaniwa alijaribiwa na Msimamizi wa Uchaguzi na kuthibitika kuwa anajua kusoma na kuandika Kiswahili na kiingereza. Aidha, amedhaminiwa na chama siasa, CHADEMA. Hivyo Tume imekubaliana na uamuzi wa Msimamizi wa Uchaguzi kuwa Mrufaniwa ni mgombea halali.
19.	Nzega Mjini	Mezza Leonard John (CUF)	Bashe, Mohammed Hussein (CCM)	Hakutoa tamko la kuheshimu na kutekeleza maadili ya uchaguzi ya mwaka 2015.	Tume imeikataa rufaa kwa kuwa mrufaniwa ametimiza sharti la kiapo cha kisheria na tamko la kuheshimu na kutekeleza Maadili ya Uchaguzi. Hivyo, Tume imekubaliana na uamuzi wa Msimamizi wa Uchaguzi kuwa Mrufaniwa ni mgombea halali.

20	Nkenge	Bagachwa Salim Abubakar (CUF)	Kamala Diodorus Buberwa (CCM)	1. Hana sifa za kuwa Mgombea Ubunge kwa kuwa wakati anajaza fomu za Tume bado alikuwa mtumishi wa serikali. 2. Hakuwasilisha Tamko la kisheria.	Tume imeikataa rufaa mrufaniwa kwa kuwa Kwa mujibu wa Waraka wa utumishi wa umma na. 1 wa 2015, Mtumishi wa umma anaruhusiwa kugombea nafasi ya ubunge na utumishi wake utakoma mara baada Tume ya Taifa ya Uchaguzi kumtangaza kuwa mgombea ubunge. Hivyo, Tume imekubaliana na uamuzi wa Msimamizi wa Uchaguzi kuwa Mrufaniwa ni mgombea halali.
21.	Ulanga	Celina Ompeshi Kombani (CCM)	Isaya Isaya Maputa (ACT – Wazalendo)	1. Hajatimiza umri wa miaka 21 2. Hawezi kusoma na kuandika 3. Si mwanachama wa chama cha siasa 4. Hakudhaminiwa na chama cha siasa kilichosajiliwa 5. Hakudhaminiwa na wapiga kula walioandikishwa katika jimbo 6. Hakudhaminiwa na idadi ya wapiga kura inayotakiwa 7. Hana Picha	Tume imeikataa rufaa kwa kuwa mrufaniwa ametimiza masharti ya kisheria. Hivyo, Tume imekubaliana na uamuzi wa Msimamizi wa Uchaguzi kuwa Mrufaniwa ni mgombea halali.
22.	Bukene	Elias Michael Machibya (CCM)	Simbi Alex Mpugi (CUF)	1. Si Mwanachama wa chama cha siasa kilichosajiliwa.	Tume imeikataa rufaa kwa kuwa mrufaniwa ametimiza masharti ya kisheria. Hivyo,

				2. Hakudhaminiwa na chama cha siasa. 3. Hakuwasilisha tamko la kisheria. 4. Hakutoa tamko la kuheshimu na kutekeleza maadili ya uchaguzi ya mwaka 2015.	Tume imekubaliana na uamuzi wa Msimamizi wa Uchaguzi kuwa Mrufaniwa ni mgombea halali
23.	Ileje	Janeth Zebedayo Mbene (CCM)	Emmanuel Amanyisye Mbuba (NCCR – Mageuzi)	1. Hana sifa ya kuwa Mgombea wa Ubunge. 2. Hakudhaminiwa na wapiga kura waliojiandikisha katika Jimbo.	Tume imeikataa rufaa kwa kuwa mrufaniwa ametimiza masharti ya kisheria. Hivyo, Tume imekubaliana na uamuzi wa Msimamizi wa Uchaguzi kuwa Mrufaniwa ni mgombea halali
24	Ileje	Emmanuel Amanyisye Mbuba (NCCR –	Janeth Zebedayo Mbene (CCM)	1. Hana sifa ya kuwa Mgombea Ubunge. 2. Hakudhaminiwa na chama cha siasa	Tume imeikataa rufaa kwa kuwa mrufaniwa ametimiza masharti ya kisheria. Hivyo, Tume imekubaliana na uamuzi wa Msimamizi wa Uchaguzi kuwa Mrufaniwa ni mgombea

		Mageuzi)		kugombea ubunge. 3. Hakudhaminiwa na wapiga kura walioandikishwa katika Jimbo. 4. Hakudhaminiwa na idadi ya wapiga kura inayotakiwa.	halali
25	Kigoma Kusini	Bidyanguze Nashon William (ADA – TADEA)	Msimamizi wa Uchaguzi (RO)	Amedhaminiwa na wadhamini 52 kwa mujibu wa sheria.	**Tume imekubali Rufaa ya mrufani kwani aliwasilisha fomu 4 za uteuzi zenye jumla ya wadhamini 52. Hivyo, Tume imemrejesha Mgombea wa ADA TADEA katika orodha ya Wagombea wa Jimbo la Kigoma Kusini .**
26	BUMBULI	DAVID JOHN CHAMYEGH (CHADEMA)	JANUARY YUSUF MAKAMBA (CCM)	Mgombea ameomba na ameteuliwa kwa nafasi mbili za ubunge na Udiwani kwa wakati mmoja.	Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura 343, katika kifungu cha 39 inasema “hakuna mtu atakayeteuliwa kuwa mgombea wa uchaguzi katika jimbo zaidi ya moja; lakini sheria haizuii

					kugombea Ubunge na Udiwani kwa wakati mmoja. Kwa maana hiyo sheria za Uchaguzi zipo kimya kuhusu mgombea kuteuliwa katika nafasi ya Ubunge na Udiwani kwa wakati mmoja. Hata hivyo, tumekuwa na “cases” za namna hii tokea Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005 na 2010 na “cases” hizi hazijapingwa na mahakama yoyote. 1. Marehemu Chacha Wangwe (2005 to 2008) Ubunge : Jimbo la Tarime Udiwani : kata ya Tarime Mjin. Charles Mwera (2008 to 2010) Ubunge: Jimbo la Tarime Udiwani: Kata ya Nyamwanga huyu alikuwa M/kiti wa Halmashauri pia wakati huohuo ni Mbunge. Vicent Nyerere (2010 mpaka 2015) Ubunge: Jimbo la Musoma Mjini Udiwani: kata ya Nkendo. Silvester Kasulumboyi (2010 mpaka 2015) Ubunge: Jimbo la Maswa Mashariki Udiwani: Kata ya Ipililo. Bunge lilirekebisha Sheria za Uchaguzi, ila sheria

					iliendela kubaki kimya juu ya suala hilo. **Hivyo, Tume imemrejesha Mgombea wa CHADEMA katika orodha ya Wagombea wa Jimbo la Bumbuli.**
27	DODOMA MJINI	KIGAILA BENSON SINGO (CHADEMA)	MAVUNDE PETER ANTONY (CCM)	Hana sifa za kuwa mgombea Ugunge kwa sababu Mgombea katika fomu yake ya uteuzi kifungu cha 5 amekiri kuwani Mkuu wa Wilaya ambaye ni Mtumishi wa Umma anatakiwa awe amejiuzulu/kuacha kazi baada ya kuteuliwa na chama chake. Kama mgombea atakuwa amekwisha acha ukuu wa Wilaya, basi kwenye fomu yake ametoa taarifa za Uongo. Kwa sababu hizo hastahili kuteuliwa kuwa Mgombea.	Tume imeikataa rufaa mrufaniwa kwa kuwa Kwa mujibu wa Waraka wa utumishi wa umma na. 1 wa 2015, Mtumishi wa umma anaruhusiwa kugombea nafasi ya ubunge na utumishi wake utakoma mara baada Tume ya Taifa ya Uchaguzi kumtangaza kuwa mgombea ubunge. Hivyo, Tume imekubaliana na uamuzi wa Msimamizi wa Uchaguzi kuwa Mrufaniwa ni mgombea halali.
28	LUDEWA	MSAMBICHAKO BARTHOLOMEO A. MKINGA (CHADEMA)	FILIKUNJOMBE DEO HAULE (CCM)	Hakutoa tamko la kuheshimu na kutekeleza Maadili ya Uchaguzi ya mwaka 2015. Hakurudisha fomu za uteuzi kwa mujibu wa Masharti yaliyowekwa na Sheria.	**Tume imekubali Rufaa ya mrufani baada ya kupitia vielelezo vilivyowasilishwa na kuona kuwa mrufani aliwasilisha fomu Na. 10 ya kuheshimu**

					nakutekeleza Maadili. Hivyo, Tume imetengua uamuzi wa Msimamizi wa Uchaguzi na imemrejesha Mgombea wa CHADEMA katika orodha ya Wagombea wa Jimbo la Ludewa.
29	KINONDONI	MTULIA MAULID SAID ABDALLAH CUF	AZZAN IDD MOHAMED CCM	Hakuna sifa za kuwa mgombea Ubunge kwa kuwa tamko la kisheria lilikamilika kwa lilisainiwa na kugongwa muhuri na Hakimu.	**Tume imeikubali rufaa ya Mrufaniwa kwa kuwa ametimiza sharti la kuapa kiapo mbele ya hakimu. Hivyo, Tume imemrejesha Mgombea wa CUF katika orodha ya Wagombea wa Jimbo la Kinondoni.**
30	MTAMA	SELEMANI SAIDI MTULUMA UPDP	MCHINJITA RASHID ISIHAKA CUF	Kwamba ameteuliwa na Chama chake. Katika fomu ya uteuzi sehemu E haikusainiwa na Wapiga Kura waliomdhamini kwa kuwa hawakupata nafasi.	Tume imekataa rufaa ya mrufani kwa kuwa hakukidhi masharti ya kisheria ikiwemo fomu kutosainiwa na wadhamini pamoja na Katibu wa Chama ambaye mrufani anadai kuwa alikuwa anaumwa. Tume inakubaliana na maamuzi ya Msimamizi wa Uchaguzi hivyo Mrufani ameondolewa

					kwenye ugombea kihalali na kisheria.
31	UKONGA	JERRY WILLIAM SILAA (**CCM)**	WAITARA MWIKABE **(CHADEMA)**	Mgombea hakudhaminiwa na Chama chake kwa kuwa fomu za uteuzi za mgombea wa CHADEMA hawana ngazi hiyo ya Uongozi.	Tume imeikataa rufa ya mrufani kwani mrufaniwa amedhaminiwa na Chama cha CHADEMA. Hivyo Tume imekubaliana na uamuzi wa Msimamizi wa Uchaguzi kuwa Waitara Mwikwabe ni Mgombea halali.
32	SENGEREMA	FRANCISCO K. SHEJUMABU (UDP)	TABASAM H. MWAGAO (CHADEMA)	Si raia wa Tanzania. Hana sifa za kuwa mgombea Ubunge. Hajui kusoma na kuandika katika Kiswahili na KiIngeReza. Hakudhaminiwa na idadi ya Wapiga Kura inayotakiwa.	Tume imekataa rufaa ya mrufani, kwa kuwa hajatoa uthibitisho kuwa mrufaniwa siyo raia wa Tanzania na kwamba hajui kusoma na kuandika. Tume imekubaliana na uamuzi wa Msimamizi wa Uchaguzi hivyo, Tabasam H. Mwagao ni mgombea halali.
33	SENGEREMA	TUMAINI MWALE KABUSINJA (NCCR – Mageuzi)	HAMIS MWAGAO TABASAM (CHADEMA)	Hana simfa za kuwa mgombea Ubunge. Hawezi kusoma na kuandika katika Kiswahili na kiingereza.	Tume imekataa rufaa ya mrufani, kwa kuwa hajatoa uthibitisho kuwa mrufaniwa hajui kusoma na kuandika. Tume imekubaliana na uamuzi wa Msimamizi wa Uchaguzi hivyo, Tabasam H. Mwagao ni mgombea halali.

34	MOSHI MJINI	KIRETI KAMASHO ISSAC (SAU)	JAPHARY RAPHAEL MICHAEL (CHADEMA)	Si raia wa Tanzania	Tume imekataa rufaa ya mrufani, kwa kuwa hajatoa uthibitisho kuwa mrufaniwa siyo raia wa Tanzania. Tume imekubaliana na uamuzi wa Msimamizi wa Uchaguzi hivyo, Japhary Raphael Michael ni mgombea halali.
35	MADABA	BUSARA LOSTOON KAISARI (ACT – Wazalendo)	Msimamizi wa Uchaguzi	Hajatibitishwa na chama kwa kuwa amethibitishwa na mtu ambaye hana mamlaka ya kuthibitisha (mwenyekiti Ngome ya Mkoa wanawake Mkoa wa Ruvuma.	**Tume imekubali Rufaa kuwa mrufaniwa amethibitishwa na Chama cha ACT Wazalendo. Imetengua uamuzi wa Msimamizi wa Uchaguzi na kumrejesha Mgombea wa ACT Wazalendo katika orodha ya Wagombea wa Jimbo la Madaba.**
36	TANGA MJINI	NUNDU OMARI RASHID (CCM)	KIDEGE HAMAD AYUBU MHAMED (ACT – Wazalendo)	Kugombea nafasi mbili tofauti kwa wakati mmoja (Ubunge na Udiwani) siyo kosa.	Sheria haimnyimi mtu kugombea nafasi mbili kwa wakati mmoja yaani udiwani na Ubunge, Tume imefikia uamuzi kuwa rufani ya Mrufani

					haina msingi, imekubaliana na uamuzi wa Msimamizi wa Uchaguzi kwa hivyo, rufaa imekataliwa.
	TANGA MJINI	NUNDI OMARI RASHID (CCM)	MUSSA BAKARI MBAROUK (CUF)	Ndugu Mussa Bakari Mbarouk amegombea nafasi mbili (Ubunge na Udiwani kwa wakati mmoja	Sheria haimnyimi mtu kugombea nafasi mbili kwa wakati mmoja yaani udiwani na Ubunge, Tume imefikia uamuzi kuwa rufani ya Mrufani haina msingi, imekubaliana na uamuzi wa Msimamizi wa Uchaguzi kwa hivyo, rufaa imekataliwa.